**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MKUTANO WA KUMI NA SITA NA KUMI NA SABA**

**YATOKANAYO NA KIKAO CHA TATU**

***(DAILY SUMMARY RECORD OF PROCEEDINGS)***

**6 NOVEMBA, 2014**

## MUTANO WA KUMI NA SITA NAKUMI SABA

## KIKAO CHA TATU - 6 NOVEMBA, 2014

**DUA**

Saa 3.00 asubuhi Mwenyekiti wa Bunge, Mhe. Mussa Azzan Zungu alisoma Dua na kuongoza Kikao.

### I: MASWALI KWA WAZIRI MKUU

Wabunge wafuatao walipata fursa ya kumuuliza Mhe. Waziri Mkuu maswali na kujibiwa

1. Mhe. Zitto Zuberi Kabwe
2. Mhe. Rajab Mbarook Mohammed
3. Mhe. Murtaza Ally Mangungu,
4. Mhe. Charles John P. Mwijage

### II. MASWALI YA KAWAIDA

Maswali yafuatayo yaliulizwa na kupatiwa majibu bungeni:-

i/ Ofisi ya Waziri Mkuu – swali Na. 29

ii/ Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) – swali Na.30

iii/ Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano) – swali Na. 31

iv/ Wizara ya Viwanda na Biashara – swali Na.32

v/ Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika – swali Na.33 na 34

vi/ Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi – swali Na. 35

vi/ Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii – swali Na. 36 na 37

**III: MATANGAZO**

i. wageni mbalimbali walitangazwa Bungeni

ii. Vikao vya kamati za Bunge ulitangazwa kufanyika katika kumbi mbalimbali.

**IV: HOJA ZA SERIKALI**

Bunge lilikaa kama Kamati ya Mipango ili kujadili na kuishauri Serilali juu Mapendekezo ya Utekelezaji wa Mpango wa Taifa kwa mwaka 2015/2016.

Wabunge wafuatao walichangia Mapendekezo ya Mpango wa Taifa kwa mwaka 2015/2016:-

1. Mhe. David Zacharia Kafulila
2. Mhe. Amina Abdullah Amour
3. Mhe. Christina Mughwai Lissu
4. Mhe. Richard M Mganga Ndassa
5. Mhe. John Momose Cheyo
6. Mhe. Mustapha Boay Akunaay
7. Mhe. Moshi Selemani Kakoso
8. Mhe. Ezekia Dibogo Wenje
9. Mhe. Harry Daffa Shekifu

10. Mhe. Capt John Damiano Komba

11. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola

12. Mhe. Pauline Philip Gekul

13. Mhe. Augustino Manyanda Masele

## V: KUSITISHA BUNGE

Mwenyekiti alisitisha Shughuli za Bunge saa 7:00 mchana hadi saa 11:00 jioni.

## VI. BUNGE KURUDIA

Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia likiongozwa na Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) na Kamati ya Mipango iliendelea na wafuatao walichangia:-

14. Mhe. Mch. Israel Yohana Natse

15. Mhe. Magdalena Hamisi Sakaya

16. Mhe. Murtaza Ally Mangungu

17. Mhe. Cecilia Daniel Paresso

18. Mhe. Dkt. Hamis Andrea Kiqwangalla

19. Mhe. David Ernest Silinde

20. Mhe. Gaudence Cassian Kayombo

21. Mhe. Kuruthum Jumanne Mchuchuli

**TAARIFA**

Mhe. Murtaza Mangungu alimpa taarifa Mhe. Kuruthumu Mchuchuli kwamba CCM haijachoka bali waliochoka ni wapinzani ndio maana wameungana taarifa ambayo Mhe. Kuruthum alikataa na aliendelea kuchangia.

22. Mhe. Kombo Khamisi Kombo

23. Mhe. Felister Aloyce Bura

**TAARIFA**

i. Mhe. Kombo Khamis Kombo alimpa taarifa Mhe. Felister Bura kwamba CCM haijaitawala watu kwa vile Watanzania walijikomboa kuhamahama na wakoloni labda kama CCM imebadilika kuwa koloni. Taarifa hii ilikataliwa na Mhe. Felister Bura aliendelea kuchangia;

ii. Wakati akichangia Mhe. Ernest Silinde alimpa taarifa Mhe. Felister Bura kwamba Rais alichaguliwa na watu milioni tano na sio milioni ishirini kama alivyosema. Taarifa hii pia Mhe. Bura aliikataa na kuendelea kuchangia;

iii. Vilevile Mwenyekiti alitoa muongozo kwa Wabunge kuvumilia kusikiliza wenzao kwani nao waliwasikiliza. Mhe. Felister Bura aliendelea kuchangia;

iv. Mhe. Rukia Kassim Ahmed naye alitoa taarifa kwa Mhe. Felister Bura kwamba barabara zinajengwa na kodi za wananchi na wala hazijengwi na CCM labda kama alikuwa ana maana nyingine. Mhe. Felister Bura alikataa taarifa hiyo.

24. Mhe. Moses Joseph Machali

**TAARIFA**

i. Mhe. Charles John Mwijage alimpa taarifa Mhe. Moses Joseph Machali kwamba suala la maadili limewekwa kwenye Katiba mpya na Mhe. Machali alikataa akisema halipo kwenye Katiba;

ii. Mhe. Mariam Kisangi pia alimpa taarifa Mhe. Moses Machali kwamba kwenye kambi yao pia wako Wabunge wana akaunti zenye sh. Bilioni mbili nao pia ni wezi lakini hawazungumzii mtu. Mhe. Machali alikataa na kutamka athibitishe kwa Kanuni ya 64 (1) (a) kwa kudai jambo hilo sio la kweli;

iii. Suala hilo Mhe. Zitto Kabwe aliliunga mkono kwa kumtaka Mhe. Mariam Kisangi athibitishe vinginevyo apelekwe kamati ya maadili. Ili Bunge lijadili mambo ya nchi;

iv. Mhe. Henry Shekifu alisema vurugu hizi zinasababishwa na UKAWA kutokana na maneno yao yasiyo na heshima;

v. Mwenyekiti alitoa mwongozo kwamba haya yote yametokea kutokana na kutochunga ndimi zao kwa pande zote na kuomba wajumbe wapime kanuni ili kuchangia kwa busara na kuwasili kuanza sasa kuchangia mpango kwa hekima na aliungwa mkono na Mhe. Pindi Chana kwamba kamati ya maadili itumike ili kanuni zisiendelee kukiukwa;

vi. Mhe. Dkt. Hamisi Kigwangallah alimpa taarifa Mhe. Moses Machali kwamba CCM haijachoka labda aseme ni baadhi ya watu sio wote. Mhe Machali alikataa taarifa hiyo.

24. Mhe. Jerome Dismass Bwanausi

25. Mhe. Prof. Kulikoyela Kanalwanda Kahigi

26. Mhe. Felix Francis Mkosamali

27. Mhe. Munde Tambwe Abdallah

**TAARIFA**

i. Mhe. George Simbachawene alimpa taarifa kwamba mtu anayekupinga kama wapinzani hawawezi kumuunga mkono na asikwazwe na maneno yao. Alikubali taarifa hii na aliendelea kuchangia;

ii. Mhe. Susan Kiwanga alisema Chadema haijapata Hati chafu bali ni query na hata CCM wana Hati chafu. Mhe. Alikataa akasisitiza Chadema kupata hati chafu na wajue uongozi sio lele mama wameshindwa kwa kula ndogo tu.

28. Mhe. Prof. Mark James Mwandosya

## VII. KUAHIRISHA BUNGE

Saa 1.45 usiku Bunge liliahirishwa mpaka kesho tarehe 7/11/14

**DODOMA**
**6 NOVEMBA, 2014**

**DKT. T.D. KASHILILAH**
**KATIBU WA BUNGE**